

Jina _____ Nambari _____

Sahihi ya mtahiniwa _____

Tarehe _____

102/1
KISWAHILI
KARATASI YA 1
INSHA
JULAI / AUGOSTI 2014
MUDA: SAA 1 $\frac{3}{4}$

KIBWEZI DISTRICT FORM 4 INTER-SCHOOLS EXAMINATIONS.
KISWAHILI
KARATASI YA 1
INSHA
MUDA : SAA 1 $\frac{3}{4}$

MAAGIZO

- (a) Andika insha mbili. Insha ya kwanza ni ya lazima.
- (b) Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizosalia.
- (c) Kila insha isipungue maneno 400.
- (d) Kila insha ina alama 20.
- (e) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi hili zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

Kijitabu hiki kina kurasa 2 zilizopigwa chapa

Geuza ukurasa

1. LAZIMA
Wewe ni mwanafunzi wa kidato cha nne. Umeombwa na mwalimu mkuu kuandika ratiba ya siku ya wazazi shuleni kwenu. Iandike.
2. Ajali za barabarani zimezidi nchini Kenya. Fafanua baadhi ya mapendekezo yanayofaa kuchukuliwa ili kupunguza janga hili.
3. Kuku mgeni hakosi kamba mguuni.
4. Andika insha itakayomalizika kwa maneno haya:
Siku hiyo nilikuja kuamini kuwa mvumilivu hula mbivu.

102/1
KISWAHILI
KARATASI YA 1
INSHA
JULAI / AUGOSTI 2014

KIBWEZI DISTRICT FORM 4 INTER-SCHOOLS EXAMINATIONS.
KISWAHILI
KARATASI YA 1
INSHA

MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

SWALI LA 1

Hii ni insha ya ratiba.

- Ratiba ni orodha au mfululizo wa mambo yanayofanyika katika shughuli au sherehe – kulingana na matendo na wakati ambapo kila tukio hutarajiwa kufanyika.
- Ratiba huenda na:
 - Shughuli za sherehe.
 - Mfuatano wa shughuli.
- Huonyesha wakati unaokusudiwa
 - Hufahamisha wanaopaswa kutenda majukumu fulani.

Utaratibu

- Andika kichwa.
- Kichwa kieleze shughuli.
- Tarehe, siku na mahali.
- Orodhesha wakati – upande wa kushoto.
- Fuatia na tukio. Matukio yapangwe kuanzia ya kwanza hadi ya mwisho.

Hoja

- (i) Kupandisha bendera / wimbo wa taifa.
- (ii) Gwaride ya wanaskauti.
- (iii) Maombi.
- (iv) Burundani kutoka kwa vikundi mbali mbali.
- (v) Hotuba.
- (vi) Zawadi.
- (vii) Shukrani.
- (viii) Moambi.
- (ix) Chamcha

SWALI LAPILI

HOJA

1. Mwendo wa kasi – Vidhibiti mwendo /mikanda ya usalama.
2. Kutotii sheria – Kuwaadhibu wakiukaji wa sheria.
3. Barabara bovu – Kuzikarabati / kuchora laini.
4. Ulevi – polisi kuwajibika na kupewa vifaa vya kupima kiwango cha ulevi.
5. Magari mabovu – kuondolewa barabarani kwa magari haya.
6. Kubeba mizigo zaidi / Abiria – Abiria kushukishwa na kufikishwa mahakamani.

Kijitabu hiki kina kurasa 7 zilizopigwa chapa

Geuza ukurasa

Tanbihi:

- (i) Mwanafunzi ataje shida kisha atoe mapendekezo.
- (ii) Atakayekosa kutoa pande mbili asahihishiwe juu ya nusu.

SWALI LA TATU

Hii ni insha ya methali. Mwanafunzi aeleze matumizi ya methali; abuni kisa kinachoafikiana na matumizi ya methali yenyewe.

Maana ya methali:- Kuku mgeni hutambuliwa kwa urahisi kutokana na kamba aliyofungwa mguuni.

Matumizi ya methali – Hutumiwa kutueleza kwamba mtu anapokuwa katika mazingira mageni hutambuliwa kwa urahisi kutokana na sura, mwendo na tabia yake.

- Lugha iwe ni ya kuvutia / atumie mbinu za lugha nyingi.
- Msamiati huwe ni wa hali ya juu. Uonyeshe ukomavu wa lugha.
- Kumbuka: Si lazima mwanafunzi aanzie na kueleza maana ya methali. Anaweza kuanza kwa kubuni hadithi / kisa au visa vinavyokueleza ukweli wa methali.

SWALI LA NNE

Hii ni insha ya mdokezo wa kumalizia. Ichukue mtindo wa insha ya masimulizi. Mtahiniwa atunge kisa kitachakuja kumalizikia na maneno aliyopewa. Ni makosa mtahiniwa kumalizia kwa maneno yake mwenyewe.

Mwili huwe wa kuvutia na wenye maudhui angalau matano. Lugha iwe ni sisimuzi, enye mvuto na iliyokomaa.

USAHIHISHAJI

Karatasi hii imedhamiria kutahini uwezo wa mtahiniwa wa kuwasiliana na msomaji na kuwasilisha ujumbe kimaandishi. Mawasiliano haya yatategemea ukwasi wa lugha ya mtahiniwa, kwa mfano, kutunga sentensi sahihi, zenye utiririko mzuri kimawazo, lugha ya kuvutia na yenye mawazo asilia. Ubunifu mwingi, na hati nadhifu. Kutegemea maagizo ya swali lenyewe na umahiri wa lugha, ni lazima kutilia mkazo mtindo, mada na uwezo wa mtahiniwa kufuata maagizo vilivyo.

Mtahini lazima asome insha yote ili aweze kukadiria viwango mbalimbali vilivyopendekezwa yaani A, B, C ama D kutegemea mahali popote pale pafaapo kuikadiria insha ya mtahiniwa.

KIWANGO CHA D

MAKI 01 – 05

1. Insha ya aina hii haieleweki kwa vyovyote, ama uwezo wa mtahiniwa wa kutumia lugha ni hafifu sana hivi kwamba mahini lazima afikirie kile anachojaribu kuandika.
2. Mtahiniwa hana uwezo wa kutumia maneno ya Kiswahili kwa njia inayofaa.
3. Lugha imevurugika, uakifishaji usiofaa na insha ina makosa ya kila aina ya kisarufi kimaendelezo, mtindo n.k

VIWANGO TOFAUTI VYA D

D- (KIWANGO CHA CHINI)

Maki 01 – 02

Insha haina mpangilio maalum na haieleweki kwa vyovyote vile, kama vile kunakili maswali au kujitungia swali na kulijibu.

D (WASTANI)

Maki 03

Utiririko wa mawazo haupo, na insha haieleweki. Makosa ni mengi.

D+ (KIWANGO CHA JUU)

Maki 04 – 05

Ingawa insha hii ina dhaifu ya Kiswahili n amakosa mengi ya kila aina, unaweza kutambua kile ambacho anajaribu kuwasilisha.

KIWANGO CHA C

Maki 06 – 10

Kiwango hiki kina makosa yafuatayo.

1. Mtahiniwa anaweza kuwasilisha mawazo yake lakini kwa kiwango kisichoeleweka kikamilifu.
2. Hana uhakika wa matumizi ya lugha.
3. Mada huwa haikukuzwa au kuendelezwa kikamilifu.
4. Mtahiniwa anaweza kupotoka hapa na pale.
5. Kujirudiarudia ni dhahiri.
6. Mpangilio wake wa kazi ni hafifu na huna mtiririko.
7. Hana matumizi mazuri ya lugha.
8. Mtahiniwa ana athari za lugha ya kwanza ambayo huonekana dhahiri, kama vile “papa” badala ya “baba”, “karamu” badala ya “kalamu”, “tata” badala ya “dada” n.k

VIWANGO VYA C

C- (KIWANGO CHA CHINI)

Maki 0 – 07

1. Mtahiniwa ana shida ya kuwasilisha mawazo yake.
2. Hana msamiati ufaao wala muundo wa sentensi ufaao.
3. Ana makosa mengi ya msamiati, hijai na matumizi mabaya ya asarufi.

C (WASTANI)

Maki 08

1. Mthainiwa anawasilisha ujumbe vizuri lakini kwa njia hafifu.
2. Hufanya makosa mengi ya sarufi.
3. Hana ubunifu wa kutosha.
4. Katika sentensi ndefu uakifishaji ake ni mbaya.
5. Ana makosa kadha ya hijai na msamiati.

C+ (KIWANGO CHA JUU)

Maki 09 – 10

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri lakini kwa njia isiyo na mvuto sana.
2. Dhana tofauti tofauti hazijitokezi kikamilifu.
3. Hutumia misemo, methali, tashbihi, tanakali za sauti n.k. kwa njia isiyofaa.
4. Utiririko wa mawazo bado haujitokezi wazi.
5. Kuna makosa machache ya sarufi na hijai.

KIWANGO CHA B

Maki 11 – 15

1. Katika kiwango hiki, mtahiniwa anaonyesha kuimudu lugha vilivyo.
2. Mtahiniwa hudhihirisha kwamba anaweza kutumia lugha kwa urahisi katika kujieleza.
3. Hutumia miundo tofauti tofauti ya sentensi vizuri.
4. Mtahiniwa ana uwezo wa kutumia lugha kwa ufasaha kama vile kuziandika sentensi kwa njia tofauti na zikaleta maana sawa.
5. Mada sharti ifuatwe na iendelezwe.

VIWANGO TOFAUTI VYA B

B- (KIWANGO CHA CHINI)

Maki 11 – 12

1. Mtahiniwa hawasilishi ujumbe wake kwa kuonyesha hoja tofauti tofauti.
2. Kuna utiririko mzuri wa mawazo.
3. Ana uwezo wa kutumia miundo tofauti tofauti ya sentensi.
4. Makosa machache yanaweza kutokea hapa na pale.

B (WASTANI)

Maki 13

1. Mtahiniwa anadhihirisha hali ya kuimudu lugha.
2. Anawasilisha ujumbe wake waziwazi kwa mawazo yanayodhihirika.
3. Mtaumizi ya lugha ya mnato huweza kudhihirika.
4. Anatumia mifano michache ya msamiati mwafaka.
5. Matumizi ya tamathali za semi yanaanza kudhihirika.
6. Mkaosa ni machache ya hapa na pale.
7. Lugha ya mnato inadhihirika.

B+ (KIWANGO CHA JUU)

Maki 14 – 15

1. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika.
2. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe wake kwa njia inayovutia na kwa urahisi.
3. Kuna makosa ya hapa na pale ambapo mtahiniwa hakudhamiria kuyafanya.
4. Uteuzi wake wa msamiati ni mzuri.
5. Sarufi yake ni nzuri.
6. Uakifishaji wake ni mzuri.
7. Lugha ya mnato inaanza kuthiirika.

KIWANGO CHA A

Maki 16 – 20

1. Mtahiniwa anadhihirisha ujuzi wa lugha yenye mnato. Ana ubunifu wa mawazo yanayodhihirika na kutiririka.
2. Ana uwezo wa kutumia tamathali za lugha ili kutoa hisia zake kwa njia iliyo bora na kwa urahisi.
3. Umbuji wake hudhihirisha ukakamavu wake kimawazo na mpangilio mzuri na hali ya kumvutia msomaji wake.

VIWANGO TOFAUTI VYA A

A- (KIWANGO CHA CHINI)

Maki 16 – 17

1. Mtahiniwa hudhihirisha ukomavu wa lugha. Ana utiririko mzuri wa mawazo kulingana na mada.
2. Huipamba lugha kwa kutumia tamathali za usemi.
3. Huzingatia matumizi mazuri ya msamiati na sarufi.
4. Makosa ya kawaida ya lugha ni nadra sana kupatikana.

A (WASTANI)

Maki 18

1. Mawazo yanadhihirika zaidi.
2. Makosa ni machache mno.
3. Hutumia lugha ya mnato.
4. Hutumia msamiati wa hali ya juu na unaovutia.
5. Sarufi yake ni nzuri.
6. Huutumia miundo tofauti tofauti ya sentensi kiufundi.
7. Hujieleza kikamilifu.

A+ (KIWANGO CHA JUU)

Maki 19 – 20

1. Mtahiniwa huwasilisha ujumbe ukulingana na mada.
2. Hutiririsha mawazo yake vizuri zaidi.
3. Hujieleza kikamilifu bila shida.
4. Hutoa hoja zilizokomaa.
5. Makosa ni machache sana – nadra kupatikana.
6. Msamiati wake ni wa hali ya juu na unaovutia

VIWANGO MBALIMBALI KWA MUHTASARI

KIWANGO	NGAZI	MAKI
A	A+	19 – 20
	A	18
	A-	16 – 17
B	B+	14 – 15
	B	13
	B-	11 - 12
C	C+	09 – 10
	C	08
	C-	06 – 07
D	D+	04 – 05
	D	03
	D-	01 – 02

USAHIHISHAJI NA UTUZAJI KWA JUMLA

Mtahini ni sharti aisome insha yote akizingatia vipengee muhimu. Vipengee hivi ni maudhui, msamiati, mtindo, sarufi na hijai.

MAUDHUI

1. Maudhui ni hoja au mambo yanayozungumziwa, kuelezewa au kuhadithiwa kwa mujibu wa mada iliyoteuliwa.
2. Maudhui ndio hasa uti wa mgongo wa insha yoyote ile.
3. Ubunifu wa mtahiniwa hukisiwa kwa kutathmini uzito wa maudhui yake kulingana na mada teule.

MSAMIATI

Msamiati ni jumla ya maneno yatumiwayo katika lugha husika. Mtahiniwa anatarajiwa kutumia msamiati unaoana na mada teule. Kutegemea ukwasi wa lugha alionao, mtahiniwa anatarajiwa kuikuza mada kwa kuifinyanga lugha kiufundi. Ni muhimu kuelewa kwamba kutokana na maendeleo na ukuaji wa teknolojia na mawasiliano, maneno mapya yanaibuka kila uchao.

MTINDO

- Mtindo unahusu mambo yafuatayo:
- Mpangilio wa kazi kiaya
- Mtiririko na mshikamano wa mawazo kiaya na katika insha nzima.
- Hati nzuri na inayosomeka kwa urahisi.
- Matumizi ya tamathali za usemi, kwa mfano, methali, misemo, jazanda na kadhalika.
- Kuandika herufi vizuri kwa mfano Jj, Pp, Uu, Ww na kadhalika
- Sura ya insha
- Unadhifu wa kazi ya mtahiniwa.

SARUFI

Sarufi ndio msingi wa lugha. Ufanisi wa mawasiliano hutegemea uwezo wa mtahiniwa wa kutunga sentensi sahihi zenye uwiano wa kisarufi. Mtahini ataonyesha makosa yote ya sarufi yaliyo katika insha anayosahihisha. Makosa ya sarufi huweza kutokea katika:

- (i) Matumizi ya alama za uakifishaji.
- (ii) Kutumia herufi kubwa au ndogo mahali pasipofaa.
- (iii) Matumizi yasiyofaa ya ngeli na viambishi, viunganishi, nyakati, hali, vihusiano na kadhalika.
- (iv) Mpangilio wa maneno katika sentensi.
- (v) Mnyambuliko wa vitenzi na majina.
- (vi) Kuacha neno linalohitajika au kuongeza neno lisilohitajika katika sentensi.
- (vii) Matumizi ya herufi kubwa :

a) Mwanzo wa sentensi

b) Majina ya pekee

- i) Majina ya mahali, miji, nchi, mataifa na kadhalika.
- ii) Siku za juma, miezi n.k.
- iii) Mashirika masomo, vitabu n.k.
- iv) Makabila, lugha n.k.
- v) Jina la Mungu.
- vi) Majina ya kutambulisha hasa wanyama wa kufugwa, kwa mfano yale ya mbwa – Foksi, Jak. Popi, Simba, Tomi na mengineyo.
- vii) Mjina halisi ya watu k.m Maria, Rutto

MAKOSA YA HIJAI / TAHAJIA

Haya ni makosa ya maendelezo. Mtahini anashauriwa asahihisha huku akiyaonyesha yanapotokea kwa mara ya kwanza tu. Makosa ya tahajia huweza kutokea katika:

- (a) Kutenganisha neno kwa mfano ‘aliye kuwa’.
- (b) Kuunganisha maneno kwa mfano ‘kwasababu’
- (c) Kukata silabi visivyo afikapo pambizoni kama vile, ‘ngan-o’
- (d) Kuandika herufi isiyofaa kwa mfano ‘ongesa’ badala ya ‘ongeza’.
- (e) Kuacha herufi katika neno kwa mfano ‘aliekujia’ badala ya ‘aliyekuja’.
- (f) Kuongeza herufi isiyohitajika kama vile ‘piya’ badala ya ‘pia’.
- (g) Kuacha alama inayotarajiwa katika herufi kama vile J, I
- (h) Kukosa kuandika kistari cha kuendeleza neno afikiapo pambizoni au kukiandika mahali pasipofaa.
- (i) Kuacha ritifaa au kuiandika mahali pasipofaa, kwa mfano ngombe, ngom’be, ng’ombe, ngo’mbe n.k.
- (j) Kuandika maneno kwa kifupi kama vile k.v., k.m., v.v., n.k. na kadhalika
- (k) Kuandika tarakimu kwa mfano 27-08-2013

ALAMA ZA KUSAHIHISHIA

- ══ Hupigwa chini ya sehemu ambapo kosa la sarufi limetokea kwa mara ya kwanza tu.
- Hupigwa chini ya sehemu au neno ambapo kosa la hijai limetokea kwa mara ya kwanza tu.
- √ Hutumiwa kuonyesha hoja inapokamilika pambizoni kushoto.
- ^ Hutumiwa kuonyesha kuachwa kwa neno / maneno.
- √ Hutumiwa kuonyesha msamiati bora. Alama hii hutumiwa juu ya neno lenyewe.
- X Hutumiwa kuonyesha msamiati usiofaa. Alama hii hutumiwa juu ya neno lenyewe.

Maelezo mafupi yanahitajika kuhusu tuzo lililotolewa . Kila ukurasa uwe na alama ya √ chini katikati ili kuthibitisha kuwa mtahini ameupitia ukurasa huo.

UKADIRIAJI WA UREFU WA INSHA

Maneno 9 katika kila msitari	ukurasa mmoja na nusu.
Maneno 8 katika kila msitari	ukurasa mmoja na robo tatu.
Maneno 7 katika kila msitari	kurasa mbili.
Maneno 6 katika kila msitari	kurasa mbili na robo.
Maneno 5 katika kila msitari	kurasa mbili na robo tatu.
Maneno 4 katika kila msitari	kurasa tatu na robo tatu
Maneno 3 katika kila msitari	kurasa nne na nusu.

Kufikia maneno	174	Insha robo.
Maneno	175 – 274	Insha nusu.
Maneno	275 – 374	Insha robo tatu.
Maneno	375 na kuendelea	Insha kamili

Jina _____ Nambari _____

Sahihi ya mtahiniwa _____

Tarehe _____

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
JULAI / AUGOSTI 2014
MUDA: SAA 2 ½

KIBWEZI DISTRICT FORM 4 INTER-SCHOOLS EXAMINATIONS.
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
MUDA : SAA 2 ½

MAAGIZO

- Jibu maswali yote.

	SWALI	UPEO	ALAMA
1	UFAHAMU	15	
2	UFUPISHO	15	
3	MATUMIZI YA LUGHA	40	
4	ISIMU JAMII	10	
	JUMLA	80	

SWALI LA 1

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali

Lugha ya Kiswahili ndio lugha muhimu katika eneo lote la Afrika Mashariki na Kati. Hii ni kwa sababu lugha hii ina nafasi ya kipekee katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda. Katika nchi hizi, Kiswahili ni lugha ya taifa. Pia, wananchi wengi wa Afrika Mashariki wanaelewa na huitumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao, hivyo kuipa lugha hii nafasi ya kipekee katika mambo muhimu kama utamaduni, siasa, na uchumi.

Wataalamu wengi wa masuala ya utamaduni wanakubaliana kwamba kwa kiasi kikubwa, lugha ni kielelezo cha utamaduni. Ukweli huo hujidhihirisha katika lugha yenyewe. Ukichunguza kwa makini lugha yoyote, utagundua kwamba ina vipengele mbalimbali vya utamaduni wa wasemaji wa lugha hiyo ambavyo vinajitokeza ndani mwake.

Vilevile, nafasi iliyonayo Kiswahili katika masuala ya siasa ni jambo lisilohitaji kupigiwa ngoma. Tangu enzi za wakoloni, lugha ya Kiswahili ilitumika kama chombo muhimu cha kuunganisha watu na kuleta umoja. Harakati nyingi ziliendeshwa kwa Kiswahili. Kwa kuwa Kiswahili ndio lugha itumiwayo na watu wengi katika Afrika Mashariki kuleta uelewano, basi ndio lugha wanasiasa hutumia katika mikutano yao.

Aidha, Kiswahili ndio lugha pekee ambayo inazungumzwa zaidi dhidi ya lugha nyingine katika maeneo ya Afrika Mashariki, Kati na Kusini ambapo zipo lugha nyingine.

Katika ukuaji wa uchumi, Kiswahili ni muhimu vilevile. Lugha ambayo inafahamika kwa watu wengi ndio ifaayo kutumiwa katika mawasiliano ya kibiashara. Tangu zamani, wananchi wa Afrika Mashariki wamekuwa wakiitumia lugha hii katika shughuli zao za kibiashara. Kiswahili kingemwezesha Mkenya kwenda Tanzania, hata vijijini, akaendesha shughuli zake za kibiashara bila taabu ya kutafuta mkalimani. Hali hii pia inajiakisi katika jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Malawi, Ngazi ja (Comoro), Burundi na Rwanda.

Siku hizi, Kiswahili kinatumika katika idhaa za nchi nyingi za ulimwengu kama vile Uchina, Afrika Kusini, Urusi, Ujapani, Ujerumani, India na nyingine ambapo Kiswahili kimepewa nafasi. Aidha, vyuo vikuu mashuhuri duniani kama vya nchini Marekani, Uingereza, Ujapani, Korea, Urusi, Uchina na kwingine sasa vinafundisha Kiswahili. Isisahaulike kuwa Kiswahili ni lugha mojawapo rasmi ya Umoja wa Afrika.

Kwa jumla, Kiswahili kinaendelea kukua kila kukicha. Kilichobaki ni kwa wakereketwa wa Kiswahili kuendelea kukieneza na kukipangia mikakati mingi inayoweza kusaidia kukiendeleza ili kiweze kusambaa kwa mapana na marefu.

Maswali

- (a) Kwa nini mwandishi anasema kuwa nafasi ya Kiswahili katika siasa “haifai kupigiwa ngoma”?

(alama 3)

(b) Kuna ithibati gani kuonyesha kuwa Kiswahili sasa kimekuwa lugha ya kimataifa. (alama 3)

(c) Unafikiri Kiswahili kina umuhimu gani? (alama 5)

(d) Eleza (alama 4)
(i) Lugha ya taifa

(ii) Lugha rasmi

SWALI LA 2

B) MUHTASARI (ALAMA 15)

Soma taarifa kisha ujibu maswali yanayofuata kutegemea maagizo.

Dunia sasa imegeuka ikilinganishwa na vile ilivyokuwa zamani. Siku hizi, jambo linapotokea popote duniani, linajulikana kwingineko kwa haraka. Hali hii imeathiri jinsi mabadiliko yanavyotokea na kuifumania jamii. Sasa, mwanafunzi anaweza kufanya maamuzi kwa haraka na kubadilisha mawazo na hivyo kufikia maamuzi hata kupitia kwa baruapepe. Hata hivyo, wakereketwa wengine wanadai kuwa hali hii imechangia pakubwa “kudhoofika” kwa tabia ya usomaji.

Katika burudani, mambo sasa ni tofauti. Zamani watu wakiwa na njia finyu za kujiburudisha lakini siku hizi zimejaa tele. Mja anaweza kuchagua kujiburudisha akiwa nyumbani kwake katika chumba cha kulala kupitia kwa mtandao. Wengi wanasema kuwa hali hii imesaidia kuwepo burudani aipendayo mtu kwa sababu ya kuwepo uteuzi. Lakini pia kuna shutuma. Hali hii inasemekana kurahisisha kasumba ya kikoloni kupitia kwa uigizwaji wa tamaduni za kigeni ikiwemo lugha.

Jamii nyingi siku hizi zimebadilisha mawazo yao na utendaji katika jamii kwa sababu ya utandaridhi. Watu wamebadilisha fikra kuhusu masuala na dhana potovu, hali ambayo imebadilisha hali ya maisha katika jamii. Dhana kama usawa wa kijinsia na mawazo ya kisasa limekuwa jambo la kawaida. Watetezi wa masuala ya kiasili wanasema kuwa hali iliyozuka imedhoofisha utamaduni wa Kiafrika, kustaarabisha watu na kuchangia kusambaratika kwa familia kutokana na kuongezeka kwa visa vya kuvunjika kwa ndoa.

Kuwepo kwa mtandao kumefanya mambo kuwa rahisi kwa njia nyingi. Lakini hali hiyo pia imechangia kuwepo kwa hali ya kuchanganyikiwa hasa miongoni mwa vijana wasioweza kujiamulia kuhusu wanayoyaona na kuyasikia. Baadhi ya watafiti pia wanasema kuwa hali hii imechangia kuwepo kwa uvivu kwa sababu ya runinga.

Kwa sababu hii pia, mabadiliko makubwa yanaendelea kutokea katika masomo huku ujanja mwingi na kutozingatiwa kwa maadili ukishuhudiwa.

(a) Eleza faida zinazotokana na mabadiliko yaliyoko katika jamii.

(Maneno 30 – 40)

(alama 6)

Nakala chafu

Nakala safi

(b) Ni matatizo gani yanayoambatanishwa na mjo wa hali ya sasa ?

(Maneno 40 – 50)

(alama 6)

Nakala chafu

Nakala safi

SWALI LA 3 – MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) Andika maneno mawili yenye silabi mwambatano ya konsonanti mbili. (alama 2)

(b) Andika sentensi hii upya kwa kutumia ‘ amba’
Basi lililogonga ng’ombe ndilo nililotaka kusafiria. (alama 2)

(c) Onyesha shamirisho kipozi katika sentensi zifuatazo. (alama 2)

- (i) Kijana amenunua baiskeli _____
- (ii) Ruth ameandika kitabu _____

(d) Weka majina yafuatayo katika ngeli zake. (alama 2)

(i) Yai _____

(ii) Mauti _____

(e) Andika sentensi zifuatazo katika kauli ya kutendwa.

(i) Paka alimla panya juzi asubuhi _____

(ii) Mzee analima shambani _____

(f) Tambulisha matumizi ya “po” katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Niliposhuka nilimwona alipokuwa amesimama.

(g) Andika sentensi hii katika hali ya udogo. (alama 2)
Alishikwa na jipu ambalo lilivimbisha kidole chake cha mguu mithili ya pera.

(h) Onyesha kielezi, kivumishi, kitenzi na nomino katika sentensi hii. (alama 4)
Watoto watatu walipeperushwa juu kwa juu na upepo mkali.

(i) Changanua sentensi ifuatayo kwa mtindo wa matawi. (alama 4)
Ruto alikimbia hadi akampata Asha.

(j) Vinyambue vitenzi vifuatavyo katika kauli ulizopewa. (alama 3)

Kitenzi

Kutendea

Kutendesha

Nya _____

Fa _____

Cha _____

(k) Ziandike tena sentensi zifuatazo kwa vinyume vya maneno yaliyopigwa mistari. (alama 2)

(i) Aliambiwa azikusanye zile mbegu.

(ii) Mbona yeye huwa amenuna kila wakati.

(l) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo. (alama 3)

(i) Fuata _____

(ii) Sheheni _____

(iii) Tahiri _____

(m) Tofautisha vitate hivi kwa kuvitungia sentensi. (alama 2)

(i) Jua _____

(ii) Chua _____

(n) Toa methali inayoafikiana na maelezo yafuatayo.

Mtu anapokuwa akipahama mahali hapaswi kupaharibu au kupatukanisha kwa kuwa huenda atahitaji kurudi hapo. (alama 2)

(o) Akifisha sentensi hii. (alama 4)

Sijui kwa nini unajisumbua bure John alimwambia Sarah hautafua dafu leo

(p) Kanusha sentensi ifuatayo. (alama 2)

Ukipita mtihani utakuwa shujaa mapema.

KIBWEZI DISTRICT FORM 4 INTER-SCHOOLS EXAMINATIONS.

**KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA**

MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

SWALI LA 1 – UFAHAMU (ALAMA 15)

1. (a) (i) Kwa sababu Kiswahili kinatumika na wanasiasa kila mahali kila kukicha kukidhi mahitaji yao.
(ii) Kwa sababu ya mvuto wa matumizi ya Kiswahili, wanasiasa wengi sasa wanakitumia.
 $1 \frac{1}{2} \times 2 = \text{alama } 3$
- (b) (i) Hatua ya umoja wa Afrika kukichakua Kiswahili kuwa lugha mojawapo rasmi katika vikao vya mikutano yake.
(ii) Kufuliwa kwa jumuiya ya Afrika Mashariki ni hatua nyingine muhimu. Moja ya mapendekezo ya jumuiya hii na serikali zake ni kuhakikisha kuwa Kiswahili kimeratibiwa kuwa lugha rasmi katika nchi hizi kumaanisha kitatumiwa katika eneo kubwa.
(iii) Kuwa inafundishwa katika vyuo vikuu vingi Marekani, Ujerumani, Uingereza, Uchina na nchi nyingine kwa onyesho kuwa kinaendelea kusambaa.
(iv) Idhaa nyingi muhimu ulimwenguni kama BBC, VOA, radio China na nyingene zinafanya matangazo ama zina vipindi kwa lugha ya Kiswahili.
 $1 \times 3 = \text{alama } 3$
- (c) (i) Kuwaunganisha raia na makabila tofauti.
(ii) Chombo cha kuwaunganisha watu wa Afrika Mashariki.
(iii) Ni kitambulishi muhimu cha utaifa na uzalendo.
(iv) Ni chombo cha mawasiliano katika kiwango cha kitaifa na hata kimataifa.
(v) Lugha ya Kiafrika, sio lugha ya kigeni kama Kiingereza ama Kifaransa.
 $1 \times 5 = \text{alama } 5$
- (d) (i) Lugha ya taifa
Lugha ya taifa na lugha inayowaunganisha watu kutoka makabila mbali mbali katika taifa ili waweze kushirikiana na kufanya kazi pamoja kukuza utamaduni wa taifa kwa manufaa ya taifa lao.
 $1 \times 2 = \text{alama } 2$

- (ii) Lugha rasmi ni lugha inayotumiwa katika shughuli za kiserikali kama vile bungeni, utawala na katika utungaji wa sheria. Lugha rasmi huwa imepewa hadhi fulani maalum na nchi fulani.

1 x 2 = alama 2

SEHEMU YA B - MUHTASARI

- (a) (i) Sasa, mwanafunzi anaweza kupata habari ama data yoyote aitakayo katika mtandao wakati wowote, hali ambayo imeathiri utoaji mafunzo.
- (ii) Watu sasa wanaweza kufanya maamuzi kwa haraka na kubadilisha mawazo na hivyo kufikia maamuzi hata kupitia kwa barua pepe.
- (iii) Katika burudani; Mja anaweza kuteua hata kujiburudisha akiwa nyumbani kwake katika chumba cha kulala kupitia mtandao.
- (iv) Jamii nyingi siku hizi zimebadilisha mawazo yake na utendaji kuhusu masuala na dhana potovu, hali ambayo imebadilisha hali ya maisha katika jamii.

3 x 2 = 6; Mt= 1, jumla 7

- (b) (i) Hali hii inasemekana kuchangia kudhoofika kwa tabia ya usomaji kutokana na utegemeaji wa mtandao.
- (ii) Hali hii inasemekana kurahisisha kasumba ya kikoloni kupitia kwa uigizwaji wa tamaduni za kigeni ikiwemo pamoja na lugha.
- (iii) Watetezi wa masuala ya kiasili wanasema kuwa hali iliyozuka imedhoofisha utamaduni wa kiafrika, kustaarabisha watu na kuchangia kusambaratika kwa familia kutokana na kuongezekaa kwa visa vingi vya kuvunjika kwa ndoa.
- (iv) Hali hiyo pia imechangia kuchanganyikiwa miongoni mwa vijana wasioweza kujiamulia kuhusu wanayoyaona na kuyasikia.
- (v) Baadhi ya watafiti pia wanasema kuwa hali hii imechangia kuwepo kwa uvivu kwa sababu ya runinga.
- (vi) Vijana kushindwa kujiamulia kuhusu wanayoyaona na kuyasikia.

Alama 1 x 6 = 6

Mtiririko alama 2

SEHEMU C. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

A. Mifano ya maneno yenye sauti mwambatano:

(i) bw – bwaga, kubwa, bweka n.k

(ii) nd – ndimu, ndoa, ndugu, ndoto, ndevu n.k

Alama 2 x 1 = alama 2

- (b) Basi ambalo liligonga ng'ombe ndilo ambalo nilitaka kusafiria. (alama 2)

Chua – Alizitoa chua kwenye mpunga
- Alichwa miguu hadi akahisi uchungu (sugua)
Lazima atunge sentensi (alama 2)

- (n) Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo.
- (o) “Sijui kwa nini unajisumbua bure.” John alimwambia Sarah “hutafua dafu leo.”
Alama $8 \times \frac{1}{2} =$ alama 4
- (p) Usipopita mtihani hautakuwa shujaa mapema.
- (q) A – Hali isiyodhihirika / hali mbalimbali k.m sisi twala, kijana acheza
Kwa : Moka kwa tatu $\frac{1}{3}$

$1 \times 2 =$ alama 2

SWALI LA NNE – ISIMU JAMII (ALAMA 10

- (i) Shuleni – wanafunzi wa shule. (alama 2)
- (ii) Takriri – Juma! Juma!
Lugha mseto – kukushow Dust
Mdokezo – Machezo ya alama za duku duku.
Nidaa – Juma ! Juma. (alama 2)
- (iii) (i) Ukosefu wa msamiati bora wa kujieleza.
(ii) Hutaka kujitambulisha na wanahirimu.
(iii) Wao hutaka kuficha mambo fulani kwa walimu.
(iv) Hutaka kuonyesha wanailewa lugha zote mbili barabara – Kiingereza na Kiswahili.
(v) Hukosa ujuzi wa kujiendeleza kwa lugha ya Kiswahili.
(vi) Wamekosa msamiati ufaao.

Zozote $6 \times 1 =$ alama 6
Mtahiniwa ataje na aeleze
Kutaja alama nusu $\frac{1}{2}$
Maelezo nusu $\frac{1}{2}$

Jina _____ Nambari _____

Sahihi ya mtahiniwa _____

Tarehe _____

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
JULAI / AUGOSTI 2014
MUDA: SAA 2 ½

KIBWEZI DISTRICT FORM 4 INTER-SCHOOLS EXAMINATIONS.
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
MUDA : SAA 2 ½

MAAGIZO

- (a) Jibu maswali manne pekee.
- (b) Swali la kwanza ni la lazima.
- (c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani Tamthilia, Ushairi na Hadithi fupi.
- (d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
- (e) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
- (f) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba karatasi zote za karatasi hii zimepigwa chapa.

Kijitabu hiki kina kurasa 4 zilizopigwa chapa

Geuza ukurasa

SEHEMU A: RIWAYA

Ken Walibora : Kidaa Kimemwozea

1. Lazima

Haki nakwambia ..., afadhali mkoloni mzungu kuliko mkoloni mweusi.

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili.

(alama 4)

(b) Thibitisha ukweli wa kauli hii.

(alama 16)

SEHEMU B : TAMTHILIA

T. Arege : Mstahiki Meya

Jibu swali la 2 au la 2

2. “Sikio la kufa halisikii dawa ... Amebadilika.

(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili.

(alama 4)

(b) Ni tamathali gani ya lugha iliyotumika katika dondoo hili.

(alama 2)

(c) Thibitisha ukweli wa dondoo hili ukimrejelea mhusika mkuu.

(alama 14)

Au

3. Kwa kurejelea tamthilia ya Mstahiki Meya kwa jumla jadili hulka za Diwani wa III.

Pamoja na umuhimu wake.

(alama 20)

SEHEMU C : FASIHI SIMULIZI

Swali la 4

(a) Eleza umuhimu wa kufanya utafiti wa fasihi simulizi nyanjani.

(alama 7)

(b) Je! Ni maandalizi gani mtafiti anafaa kufanya kabla ya kwenda nyanjani.

(alama 7)

(c) Eleza baadhi ya vikwazo ambavyo mtafiti anaweza kukabiliana navyo wakati anapofanya utafiti.

(alama 6)

SEHEMU D : HADITHI FUPI

Damu Nyeusi (Ken Walibora)

5. (a) Eleza ni kwa nini Ken Walibora amechanganya lugha katika hadithi hii.

(alama 2)

(b) Eleza sifa zozote tano za Fikirini kama zinavyojitokeza katikaa hadithi.

(alama 10)

(c) “Nyumbani ni nyumbani ingawa pangoni” Eleza ukweli wa methali hii ukimrejelea Fikirini.

(alama 8)

Au

6. **KANDA LA USUFI na (Rhoda Nyaga)**

Fafanua mada ya Kanda la Usufi katika hadithi ya Kanda la Usufi.

(alama 20)

SEHEMU YA E : USHAIRI.

Jibu swali la 7 au 8

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

1. Kuzimu wenda kuona, kila mdharau chake
Cha kwake akakikana, kutamani cha mwenzake
Fahamu anayo lana, mpiga chake mateke
Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona.
2. Siringe na kujivuna, chako ukakipa teke
Unavunja lako jina, ili watu wakucheke
Ana lana kwa Rabuka, kila mdharau chake
Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona.
3. Chako japo si cha mana, kibaya mtu ni chake
Kitunze na kukinena, na ukiye hadhi yake,
Kisifu ukiye jina, kipambe na kipambike,
Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona.
4. Awe Fatu na Amina, au Asha ndugu yake,
Katu hawatafanana, kila mtu hadhi yake,
Kila mjuzi wa mana, huwa hadharau chake,
Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona.
5. Tama naomba amina, kilicho chetu tushike,
Kidumu na kulingana, na tukipe hadhi yake,
Ana lana kwa Rabuka, kila mdharau chake
Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona.

Maswali

- (a) Lipe shairi hilo kichwa mwafaka. (alama 2)
- (b) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 5)
- (c) Katika ubeti wa tatu uhuru wa mtunzi unadhohirika vipi? Tolea mfano kauli yako. (alama 4)
- (d) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- (e) Mtunzi ana maana gani anaposema.
 - (i) Kuzimu enda kuona. (alama 2)
 - (ii) Ana lana kwa Rabuka. (alama 2)
 - (iii) Kipambe na kipambike. (alama 1)

8. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

TOSHEKA

1. Mwanaadamu tosheka, tosheka na lako fungu,
Ingawa dogo ridhika, akupalo bwana Mungu,
Punguza mno kutaka, si haki sahibu yangu,
Mwanadamu tosheka, akupacho Bwana Mungu.
2. Tosheka na upatacho, kisha himidia Mungu,
Na kiwe kidogo hicho, hilo ndilo lako fungu,
Usikondolee jicho, kilicho ndani ya mvungu,
Mwanadamu tosheka, akupacho Bwana Mungu.
3. Moyo siupe msiba, kujaa kizungu zungu,
Kuona Juma Kashiba, ukakushika uchungu,
Mabaya ukagabeba, ukazusha kila jungu,
Mwanadamu tosheka, akupacho Bwana Mungu.
4. Kama ndogo hali yako, alokupa bwana Mungu,
Usimwadui mwenzako, alopata kubwa fungu,
Lipi kosa lako kwako, hata waona uchungu,
Mwanadamu tosheka, akupacho Bwana Mungu.
5. Mwanaadamu kinai, kinai na lako fungu
Usiwe mtu adui, ili uongeze fungu
Jambo hili halifai, kupata kitu ni Mungu,
Mwanadamu tosheka, akupacho Bwana Mungu.

Maswali

- (a) Eleza ujumbe wa shairi hili. (alama 4)
- (b) Katika ubeti wa 3 mtunzi anatushauri moyo wetu tusiupe msiba. Kwa nini? (alama 3)
- (c) Eleza maana ya mafungu yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi.
 - (i) Kilicho ndani ya mvungu.
 - (ii) Kupata kitu ni Mungu. (alama 4)
- (d) Bainisha toni ya shairi hili. (alama 2)
- (e) Fafanua kwa kutoa mifano miwili ya mbinu alizotumia mskari kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika shairi hili. (alama 4)
- (f) Eleza umuhimu wa kiishio cha shairi. (alama 3)

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
JULAI / AUGOSTI 2014

KIBWEZI DISTRICT FORM 4 INTER-SCHOOLS EXAMINATIONS.

**KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI**

MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

SEHEMU A : RIWAYA

1. Ken Walibora : Kidagaa Kimemwozea.

- (a) - Maneno haya yalisemwa na Matuko.
- Alikuwa akiwaeleza Amani na Imani.
- Walikuwa Seli katika kituo cha polisi.
- Alisema maneno haya kwa sababu ya mateso ambayo walipata kutoka kwa viongozi waafrika ambao walishika hatamu baada ya mkoloni kuondoka.
- Matuko alikuwa amekamatwa baada ya kuzusha vurugu katika mkutano wa Nasaba Bora na Imani walishikwa kwa kumuua mtoto uhuru.

Zozote 4 x 1 = alama 4

(b) Ukweli wa kauli hiyo

- (i) Ingawa mkoloni mzungu aliwapokonya mashamba aliwaacha wakiwa hai. Nasaba Bora aliwapokonya mashamba kisha akawaua mf. Mamake Amani na babu yake Imani.
(ii) Wakati wa mkoloni mzungu nyumba za wafanyakazi zilikuwa zimejengwa na kutunzwa vizuri.
- Nasaba Bora alipuuza vibanda za wafanyakazi.
(iii) Mkoloni mzungu aliwatuza askari wake walioenda vitani mf. Majununi alipewa shamba.
- Viongozi waafrika waliwaacha mashujaa wao mfano Matuko kudharauliwa na kukosa makao /chakula.
(iv) Wakati wa mkoloni mzungu wafanya kazi walihifadhi pesa mfano Mwinyi hatibu, na baadaye wakajinunulia mashamba yao wenyewe.
- Wakati wa mkoloni mwafrika wafanyakazi walilipwa mshahara duni wakawa hawawezi kujikimu.
(v) Majununi alitunza nyumba yake.
- Nasaba Bora aliachilia ile nyumba ikawa kama mahame.
(vi) Mbwa walituzwa wakati wa mkoloni mzungu.
- Nasaba Bora aliwaachilia mbwa ugonjwa na wakaanza kuuma watu.
(vii) Wazungu hawakutuma majambazi kwenda kuwaua watu wasio na hatia.
- Nasaba Bora hakujali chochote alimua mamke Imani na kuchoma nyumba yao.
- Kila hoja ni lazima iwe na pande mbili

Mkoloni – 2 alama

Mkoloni mwafrika – 2 alama

Kijitabu hiki kina kurasa 5 zilizopigwa chapa

Geuza ukurasa

SEHEMU B : TAMTHILIA

T. Arege: Mstahiki Meya

2. (a) - Maneno haya yalisemwa na Diwani III.
- Alikuwa akimwambia Daktari Siki.
- Walikuwa nyumbani kwa Diwani III.
- Diwani III alikuwa anazungumza jinsi Meya amekataa kusikiliza ushauri wake.

Zozote $4 \times 1 = 4$

(b) Methali mf. Sikio la kufa halisikii dawa. (alama 2)

(c) Mhusika mkuu ni Meya

- (i) Meya anaonywa kuhusu ukosefu wa dawa
Anawadaganya kuwa ameagiza dawa
- (ii) Meya anashauriwa kuhusu Vifo.
Anapuuza anasema huyo mmoja tu.
- (iii) Meya anaonywa kuwa baraza halina pesa. Yeye anapuuza na hata anawaongezea madiwani mshahara.
- (iv) Meya anajua kwamba kuna mgomo.
Anapuuza mgomo mpaka wageni wakawa hawawezi kuwasili.
- (v) Sosi anajua hali ya elimu ni duni nchini Cheneo. Anapuuza na kupeleka watoto wake ng'ambo.
- (vi) Sosi anajua hali ya matibabu / Afya ni mbaya nchini Cheneo. Yeye anampeleka mke wake ng'ambo baadala ya kuboresha matibabu.
- (vii) Meya anaelewa kuwa mazao yamedidimia. Analetewa mayai madogo sana kwa kuwa kuku hawana chakula. Anawalaumu wakulima na hata kusema wasimletee mayai tena.
- (viii) Meya anaelewa kuwa baraza halina pesa. Anatoa amri madiwani wasilipe kodi licha ya kushauriwa na mtaalamu wa uchumi.
- (ix) Kandarasi Meya anajua kuwa Bili sio mtaalamu wa mambo ya uchumi lakini anakubali ushauri wake kuhusu kandarasi.
- (x) Meya anakubali ushauri wa Diwani I kwamba watumie propaganda badala ya kushughulikia matatizo ya jamii.

Hoja zozote $7 \times 2 = 14$

3. Hulka za Diwani III

- (i) Mtetezi wa Haki. Mf. Anawatetea wafanyakazi.
- (ii) Hafi moyo Mf. Anasisitiza kwamba atazidi kwenda kwa Meya tena na tena hadi akubali.
- (iii) Ni mzalendo Mf. Anawatetea wananchi waliomchagua.
- (iv) Ni jasiri Mf. Anapinga kuundwa kwa kamati. Anasema lengo la kamati hizo ni kutumia pesa zaidi ambazo hazipo.
- (v) Ni mwenye utu Mf. Anaona uchungu kwenda kazini na kuona watu wakiteseka.
- (vi) Nimwenye hekima Mf. Anamweleza Siki kuwa hata siasa zinahitaji watu waliosoma kama yeye.
- (vii) Ni mwanamapinduzi Mf. Anaambia Siki kwamba watu wote wanafaa kuungana na kutoa uozo katika jamii.
- (viii) Ni mkweli Mf. Anajaribu kuwaeleza madiwani wenzake wawatete wananchi waliowachagua na kuwatendea haki.

Hoja zozote $6 \times 2 = 12$

UMUHIMU

- (i) Ni kielelezo cha mtetezi wa haki mfano anawatetea wananchi wanaonyanyaswa.
- (ii) Ni mfano wa kiongozi bora Mf. Kutumikia waliomchagua sio kutetea viongozi.
- (iii) Ni kielelezo cha uwajibikaji Mf. Anasema baraza halina pesa.
- (iv) Kielelezo cha uzalendo mf. Hafi moyo.
- (v) Kielelezo cha utu. Mf. Aliacha kwenda kazini kwa sababu aliona uchungu watu wakiteseka.

Zozote $4 \times 2 = 8$

4. (a) Umuhimu wa kufanya utafiti wa fasihi simulizi Nyanjani.
- (i) Unamwezesha mtafiti kujionea / kushuhudia matukio katika hali yake ya kimsingi.
 - (ii) Mtafiti huweza kupokea ujumbe moja kwa moja kutoka kwa jamii husika.
 - (iii) Humpa mtafiti fursa ya kushiriki / kujihusisha na tukio.
 - (iv) Mtafiti huweza kupokea ujumbe kwa lugha ya wenyeji.
 - (v) Utafiti unasaidia kutunza na kuhifadhi turathi za jamii.
 - (vi) Utafiti unasaidia matayarisho ya uchapichaji wa fasihi simulizi na tanzu zake.
 - (vii) Humwezesha mtafiti kupata taswira / toni / mguso / hisia za watendaji wa F.S
 - (viii) Humwezesha mtafiti kunasa sauti za matukio.
 - (ix) Utafiti wa F.S unaendeleza taaluma ya F.S.

Zozote $7 \times 1 =$ alama 7

- (b) Maandalizi kabla ya kwenda nyanjani.
- (i) Kuteua / kuchagua mada ya kutafitia.
 - (ii) Kutambua shabaka /lengo la utafiti.
 - (iii) Kuamua / kuchagua mbinu / vifaa vya kufanyia utafiti.
 - (iv) Kuchagua / kuamua jamii / mahali pa kufanyia utafiti.
 - (v) Wasiliana na viongozi ili kupata kibali.
 - (vi) Kutafuta msaidizi anayefahamu jamii husika.
 - (vii) Tayarisha usafiri.
 - (viii) Hakikisha vifaa vyote vya kurekodi viko sawa.
 - (ix) Fanya bajeti ya matumizi.

Zozote $7 \times 1 =$ alama 7

VIKWAZO

- (i) Hali ya anga isiyotegemeka mf. Mvua, ukame.
- (ii) Matatizo ya usafiri mf. Kukosa magari.
- (iii) Kaharikiwa na vifaa vya utafiti.
- (iv) Shida ya lugha ya kuwasiliana na jamii husika.
- (v) Uhaba wa fedha za kugharamia utafiti.
- (vi) Kutomaliza utafiti.
- (vii) Vikwazo vya kijamii mf. Imani.
- (viii) Kushukiwa kuwa jasusi.
- (ix) Kunyimwa kibali.
- (x) Ukaba wa vifaa.

Zozote $6 \times 1 =$ alama 6

SEHEMU D : HADITHI FUPI

5. (a) (i) Ken Walibora amechanganya lugha kwa sababu mandhari ya hadithi ni marekani.
(ii) Alitaka kutupa hali halisi ya mambo.
(iii) Kutoa hisia za watumiaji.

Zozote 2 x 1 = alama 2

(b) Sifa za Fikirini

- (i) Msomi – Mfano ameenda Marekani kwa masomo.
(ii) Mwenye hekima mf. Ingawa anaulizwa maswali ya kijinga anayajibu kwa werevu mwingi.
(iii) Mvumilivu Mf. Anaendelea na masomo katika hali ngumu ugenini.
(iv) Mzalendo mf. Alisisitiza kuwa angerudi nyumbani baada ya masomo.
(v) Mwoga mf. Alilia alipoelekezewa kisu pamoja na bunduki na BO6
(vi) Anashawishika kwa haraka mf. Alimfuata Fiona bila kufikiria wanaenda wapi.
(vii) Ana maadili mf. Alikataa kufanya mapenzi na Fiona.

Hoja zozote 5 x 2 = alama 10

- (c) (i) Hali ya anga Marekani ni tofauti na ya Afrika mf. Marekani kuna theluji nyeupe na baridi ya ajabu. Afrika kuna joto.
(ii) Joto wakati wa joto kule Marekani huwa jingi mpaka watu wanatembea nusu uchi.
(iii) Vyakula. Mtu akiwa Marekani anatamani vyakula vya nyumbani kama ugali, matoke, mihogo n.k.
(iv) Wasichana mf. Fikirini alikumbuka wasichana wa kwao kama Wakamba , Wanyankole, Wahaga n.k
(v) Ndoa . Ndoa za Marekani ni za mkataba lakini za Afrika ni za kudumu.
(vi) Ubaguzi. Afrika hakuna ubaguzi kama Marekani. Kuna mapenzi.

Zozote 4 x 2 = alama 8

6. (i) Kitu cha kumtuliza mja wakati ana mahangaiko.
(ii) Masazu alienda shule ya wasichana ya Askofu Timotheo kwa nia ya kumtafuta msichana ambaye angefanya urafiki naye.
(iii) Barua aliyopokea Sela kutoka kwa Masazu ilikuwa imepakwa marashi na kujaa maneno matamu yaliyomtuliza Sela roho.
(iv) Baada ya kujipaka mja mzito Sela aliandikiwa barua na Mazazu ya kumwambia kuwa yajayo yapokee.
(v) Masazu alimpata Sela na kuanza urafiki naye ili kutuliza ashiki zake za mwili.
(vi) Kitoto – Sela alijifungua kitoto chake Wadogo. Mtoto ni kitulizo kwa mwanadamu.
(vii) Sela aliweza kurudi shuleni na kuendelea na masomo yake.
(viii) Sela aliendelea kuishi na Masazu, sabuni ya roho yake, kule alilokuwa anafanya kazi katika shamba la mkongwe.
(ix) Sela alienda kumwita mtoto wake Kadogo. Hii ni kwa sababu alibaki peke yake nyumbani Masazu alipoenda kazini.
(x) Alimtaka Kadogo aje awe kanda la usufi kwake.

Hoja zozote 10 x 2 = alama 20

USHAIRI

7. (a) - Kila mdharau chake
- Tunza kilicho chake
(alama 2)
- (b) (i) Kila mshororo una mistari minne.
(ii) Vina katika mishororo ya kwanza miwili katika kila ubeti vinafanana lakini mishororo inayofuata vinabadilika.
(iii) Kiishio kinarudiwarudiwa.
(iv) Kila mshororo una mizani 16
(v) Shairi lina beti 5
(vii) Kila mshororo una vipande viwili.
Zozote 5 x 1 = alama 5
- (c) Inkisari – mf. Hana
Kuboroga sarufi mf. Kibaya mtu ni chake
Kutaja 1 mfano 1
(2 x 2 = alama 4)
- (d) - Hata kama ni ndugu waliozaliwa tumbo moja.
- Daima hawawezi kuwa sawa kwa maana kila mmoja ana riziki yake.
- Kila mtu mwenye kujiheshimu hawezi kudharau kile kilicho chake.
- Kwa maana yule mwenye kudharau kilicho chake mwishowe hujuta.
4 x 1 = alama 4
- (e) Kuzimu enda kuona – hujuta baadaye. (alama 2)
Ana lana kwa Rabuka – ana laana kwa Mungu. (alama 2)
Kipambe na kipambike – kitunze. (alama 1)
8. (a) (i) Shairi hili ni wasia kwa mwanadamu atosheke na alichopewa na Mungu.
(ii) Linashauri mwanadamu asionee wivu akiba ya jirani.
(iii) Wasiwe na uchungu wakiona wenzao wametosheka.
(iv) Wasitamani kuchukua fungu la wenzao.
(v) Mungu ndiye anayepeana.
(vi) Anatushauri tupunguze tama.
Zozote 4 x 1 = alama 4
- (b) - Kwa sababu utajaa kizungu zungu.
- Watashikwa na uchungu.
- Watabeba mambo mengi mabaya.
- Watazusha ghasia.
Zozote 3 x 1 = alama 3
- (c) (i) Kilicho ndani ya mvungu – Hazina / akiba / utajiri
- Kilichofichwa (alama 2)
- (ii) Kupata kitu ni Mungu – Mungu ndiye mpaji. (alama 2)
- (d) Toni ya kushauri wanadamu / Toni ya kuasa. (alama 3)
- (e) - Kiishio kinasisitiza kwamba binadamu anafaa kutosheka na kile alichopewa na Bwana.